

*Mulika, Na. 43 (2), 257-276
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Uhusiano wa Wapemba na Wamakonde: Hoja za Kihistoria

Pendo Mwashota¹

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa
na

Mussa Hans²

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t2.4>

Ikisiri

Makala haya yanahu uhusiano wa Wapemba na Wamakonde kwa kuegemea katika hoja za kihistoria. Data za utafiti uliozaa makala haya zimekusanywa kwa njia ya usaili, hojaji na ushuhudiaji katika maeneo ya Kisiwa cha Pemba na katika mkoaa wa Mtwara. Uchambuzi wa data umeongozwa na nadharia mbili ambazo ni Nadharia ya Mwachano na Makutano ya lugha za Kibantu na Nadharia ya Isimu Historia Linganishi. Data za makala haya zimechambuliwa kwa mkabala wa kitaamuli Matokeo ya utafiti uliozaa makala haya yanaonesha kuwa kuna uhusiano wa karibu wa kihistoria baina ya Wapemba na Wamakonde unaotokana na sababu mbalimbali kama vile kuhamahama, kukimbia vita, kuoana na suala la shughuli za uchumi na biashara.

1.0 Utangulizi

Uhusiano baina ya jamii mbalimbali ulimwenguni ni suala ambalo limefanyiwa kazi na wanazuoni mbalimbali ulimwenguni. Miongoni mwa wanazuoni hao ni Fox (1995) na Hock na Joseph (1996) ambao wameangalia uhusiano baina ya jamiilugha za Ulaya. Kwa upande wa Afrika, kuna wanazuoni mbalimbali waliofanya uchunguzi wa uhusiano baina ya jamiilugha mbalimbali zikiwamo jamiilugha za Kibantu kwa mfano Greenberg (1955) na Guthrie (1948, 1967, 1970 na 1971). Halikadhalika kwa upande wa Tanzania wapo wanazuoni waliofanya utafiti wa uhusiano baina ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu kwa mfano Massamba (2007), Hans (2014) na Mwashota (2019). Hans (2014) amechunguza uhusiano uliopo baina ya Wapemba, Watumbatu na Wamakunduchi kwa kuangazia kipengele cha msamiati.

Aidha, Mwashota (2019) kwa upande wake amefanya utafiti kuhusu uhusiano wa kimsamiati na kihistoria baina ya Kipemba, Kimakunduchi na Kimakonde na

¹ Baruapepe: pendo.mwashota@udsmt.ac.tz

² Baruapepe: hansmussa@udsmt.ac.tz

mchango wake katika maendeleo ya Kiswahili. Katika tafiti hizi mbili uhusiano baina ya jamiilugha ya Kipemba na Kimakonde kimsamiati umedokezwa kwa kueleza kwamba wazungumzaji wa Kipemba wanatumia nazali /n/ mahali pa nazali /m/ kwa mfano katika neno mtu wao husema **ntu** wakati wa uzungumzaji kama ilivyo kwa wazungumzaji wa Kimakonde ambao nao hutumia nazali /n/ mahali pa nazali /m/ kwa mfano mwanamke wao husema *mwananke*.

Katika makala haya uhusiano uliojadiliwa ni wa kihistoria unaowahuju Wapemba na Wamakonde. Katika kujadili uhusiano huu kuna mambo mbalimbali yamezingatiwa ikiwa ni pamoja na asili ya majina ya Kipemba na Kimakonde. Pia, chimbuko la Wapemba na Wamakonde limefafanuliwa. Katika kuangalia uhusiano baina ya Wapemba na Wamakonde kihistoria kumbukumbu mbalimbali za kihistoria zimetumika kutoka katika matini mbalimbali, watoataarifa ambao ni wazungumzaji wa Kipemba na Kimakonde wametumika na uhusiano wa kimnasaba umezingatiwa.

2.0 Nadharia

Utafiti uliozaa makala haya uliongozwa na nadharia mbili yaani, Nadharia ya Mwachano na Makutano ya Lugh za Kibantu na Nadharia ya Isimu Historia Linganishi. Mwachano na Makutano ya luga za Kibantu ni mtawanyiko na makutano ya jamiilugha na ndiyo sababu ya mabadiliko mbalimbali ya vipengele vya kiisimu katika jamiilugha hizo (Massamba, 2007). Aidha, mabadiliko hayo ndiyo chanzo cha kutokea kwa tofauti za usemajii. Massamba anaendelea kufafanua zaidi kuwa, jamiilugha zinaweza kuachana kiisimu kutokana na sababu za kijamii na/au kiuchumi. Wakati huohuo jamii hizi zinaweza kujikuta ziko katika makutano kutokana na sababu hizohizo za mwachano. Hali hii huweza kutokea baada ya miaka mingi kupita. Kwa mfano, watu wanaweza kuhama na kwenda maeneo mengine kwa ajili ya kutafuta maisha bora na ardhi yenyre rutuba kwa ajili ya kilimo ama malisho kwa ajili ya mifugo. Kwa upande mwingine, jamii iliyoachana kwa muda mrefu inaweza kujikuta iko katika makutano baada ya miaka kadhaa kupita. Jambo la msingi la kuzingatia ni kwamba mchakato wa mwachano na/au makutano unaweza kuchukua muda mrefu hata maelfu ya miaka.

Athari za mwachano na makutano ya kiwakati zimefafanuliwa pia na Massamba (2007) na Hans (2014); ambao wamefafanua athari za mwachano na makutano kiwakati kwa wazungumzaji wa lahaja mbalimbali za Kiswahili. Katika ufanuzi wao wanaeleza kuwa wazungumzaji lugha moja wanapotengana kwa muda mrefu, hufika wakati wakatofautiana katika matumizi ya lugha yao hatimaye hujikuta wanazungumza lahaja tofauti na utengano unapokuwa wa muda mrefu huweza kujikuta wanazungumza lugha tofauti.

Nadharia ya Mwachano na Makutano inafafanuliwa kwa uwazi zaidi na nadhariatete ambayo Massamba (2007) ameiita Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali. Kwa mujibu wa nadhariatete hii, lugha za jamiilugha mbili zenye

uhusiano wa kinasaba na zenyе mawasiliano ya karibu (ndugu) zinaweza kuathiriana zaidi kuliko lugha za jamiilugha ambazo hazina uhusiano huo wa kinasaba au mawasiliano ya karibu (ndugu wa mbali). Kinachosisitizwa hapa ni kwamba, ili lugha ziweze kuwa na kiwango kikubwa cha kuathiriana kimsamiati, ni lazima lugha hizo ziwe na sifa zote mbili za uhusiano wa kinasaba na mawasiliano ya karibu kwa wanajamiilugha wake kwa kipindi kirefu.

Hans (2014: 154) mbali na kuonesha ufaafu wa Nadharia ya Mwachano na Makutano ya Lughya za Kibantu, pamoja na Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali ameiboresha nadhariatete kwa kupendekeza kuongezwa kwa dhana ya Ndugu wa Karibu. Pendekezo lake linatokana na matokeo ya utafiti alioufanya Zanzibar kuhusu uhusiano wa lahaja za Kiswahili.

Suala la Mwachano na Makutano limewahi kujadiliwa pia na Nurse na Spear (1985); Nurse na Hinnebusch (1991); Nurse (1997) na Nurse na Heine (2008) ambao wanasema kuwa wakati wa mtawanyiko, Wabantu walisambaa kuelekea katika maeneo tofautitofauti. Wengine walielekea pwani ya Afrika Mashariki na kufanya makazi yao kandokando ya pwani hasa pale walipoona panawafaa.

Msambao wa makazi wa Wabantu wakiwamo Waswahili kama ilivyo misambao mingine, ulichukua muda mrefu. Kwa mfano, Massamba (2007; 2017) ameandika kuhusu mgawanyiko wa jamii ya Waswahili kama ilivyo kwa jamii nyingine za Kibantu. Amefafanua pia namna hizi zinazoitwa lahaja za Kiswahili zilivyoanza ambapo kwa mtazamo wake hizi tunazozita lahaja za Kiswahili zilianza kama lugha kamili zinazojitegemea.

Wazungumzaji wa Kimakonde na Kipemba kwa upande mwingine wanaweza kuchukuliwa kuwa na ukaribu kijamii na hata kijiografia kutokana na chimbuko lao na kwa kiasi fulani jiografia yao kwa kuzingatia kwamba wote wako katika maeneo ya pwani ya bahari ya Hindi. Utafiti huu umetumia Nadharia ya Mwachano na Makutano na Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali katika uchambuzi wa data zinazohusu uhusiano wa Wapemba na Wamakonde. Aidha, matokeo ya utafiti yametusaidia kutoa hitimisho la uhusiano wa kihistoria baina ya Wapemba na Wamakonde.

Vilevile, nadharia hii imesaidia kufanya kazi madai ya jumla yaliyotolewa na baadhi ya wanaismu kama vile Chum (1994), Hans (2014) wanaoeleza kuwa, kuna umuhimu wa kuchunguza uhusiano uliopo baina ya lahaja za Kiswahili na lugha za Kibantu. Hivyo, utafiti uliozaa makala hayani sehemu ya utekelezaji wa pendekezo hili kwani uhusiano huo umewekwa bayana katika makala haya kuitia uhusiano baina ya Wapemba na Wamakonde.

Nadharia ya pili iliyotumika katika utafiti huu ni Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi. Nadharia hii inahusisha taaluma mbili tofauti za isimu, yaani isimu historia na isimu linganishi. Wakati isimu historia inashughulikia mabadiliko na

maendeleo ya lugha kiisimu, isimu linganishi inahusika na kulinganisha lugha mbalimbali zinazohusiana kwa viwango tofautitofauti. Ulinganishi huu huweza kuangaliwa katika vipengele mbalimbali via kiisimu na

pengine kihistoria. Vipengele via kiisimu ni kama vile sauti, maumbo ya maneno, miundo ya maneno, msamiati na maana. Makala haya yameegemea zaidi katika kipengele cha kihistoria hususan kulinganisha uhusiano baina ya Wapemba na Wamakonde kwa hoja za kihistoria.

Maandiko mbalimbali kama vile ya Fox (1995: 17-19), Joseph na Hock (1996: 35-41), Beeks (2011: 13-14), na Bowern na Evans (2015: 47) yanaonesha kuwa mwanzilishi wa Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi ni William Jones mwaka 1786. Hata hivyo, Luraghi na Bubenik (2010: 7-8) wanasema kuwa kabla ya William Jones kuna mwanaisimu mwingine aitwaye Jesuit Janos Sajnovics 1770, aliywahi kuzungumzia suala la isimu historia-linganishi. Sajnovics alilinganisha mofimu ambatani za lugha za Kilapu “Lapp” na Kihangaria, na kugundua kuwa zinafanana. Hata hivyo, si nia ya makala haya kuzungumzia yupi hasa ni mwasisi wa nadharia hii, bali kuonesha namna nadharia hii inavyoweza kutumika katika kuchambulia na kuwasilisha data za utafiti wa makala hii.

Jones alianzisha nadharia hii kupitia mhadhara wake uliohusu lugha ya Kisanskriti ambapo aligundua kuwa Kiyunani, Kilatini na Kisanskriti zinaelekeea kuwa na chimbuko moja. Pia, lugha hizo zilionekana kuhusiana na Kipashia, Kigothiki na Kiseltiki/Kikeltiki. Msingi mkuu wa Nadharia ya Isimu Historia Linganishi ni kuangazia uhusiano baina ya lugha na lugha, lugha na lahaja au lahaja na lahaja kiisimu na kihistoria. Kwa upande wa makala haya Nadharia ya Isimu historia-linganishi imesaidia kuongoza ufanuzi wa uhusiano baina ya Wapemba na Wamakonde kihistoria. Aidha, suala la ulinganishi wa kihistoria baina ya wazungumzaji wa lugha/lahaja si geni kwa sababu limewahi kufafanuliwa na Dante Alighieri katika miaka ya 1265-1321³. Ulinganishi wa uhusiano baina ya kundi husika la wazungumzaji hufanyika kwa lengo la kufahamu chimbuko la wazungumzaji wanaohusika.

3.0 Methodolojia

Utafiti uliozaa makala haya umefanyika uwandani. Maeneo yaliyoteuliwa kukusanya data ni pamoja na maeneo ya Kisiwa cha Pemba katika maeneo ya Kisiwa Panza, Shamiani, Kojani. Maeneo haya yalichaguliwa kwa sababu ni maeneo yanayozungumzwa Kipemba cha asili. Kwa upande wa Mtwara data zilikusanya katika maeneo ya Msimbati, Mgao, Mkungu, Mikindani na Msanga Mkuu. Jumla ya watoataarifa waliohusika katika utafiti huu ni 20 kwa maana ya kwamba Kisiwa cha Pemba walikuwa 10 na mkoa wa Mtwara watoataarifa walikuwa 10. Mbali na mambo mengine, watafiti walizingatia umri na uzoefu wa

³ Kwa ufanuzi zaidi tazama Mwashota (2019:97)

watoataarifa kwa lengo la kupata data za uhusiano wa kihistoria baina ya Wapemba na Wamakonde. Aidha, uchambuzi na uwasilishaji wa data umetumia mkabala wa kitaamuli yaani mkabala unaotumia njia ya maelezo na sio takwimu (Enon, 1998 na Creswell, 2014).

4.0 Matokeo na Mjadala

Sehemu hii inafafanua matokeo ya utafiti uliozaa makala haya pamoja na mjadala kama yanavyofafanuliwa katika vipengele vifuatavyo:

4.1 Asili ya Jina la Pemba

Watoataarifa wengi kutoka Pemba wana mtazamo kwamba jina Pemba limeanzia Tanzania Bara wakihuisha na eneo linaloitwa Pemba Bay⁴. Madai ya watoataarifa hawa ni kwamba, kulikuwa na watu amba walitokea Tanzania Bara wakahamia Pemba na katika harakati za kuienzi sehemu waliyotokea wakajikuta wanalita eneo walilofikia Pemba. Maelezo ya watoataarifa hawa yanaelekeana na maelezo ya baadhi ya watoataarifa kutoka Mtwara mathalani Msanga Mkuu. Watoataarifa wengine walisema kwamba watu waliohama kutoka Msumbiji eneo la Pemba kila walipofika walipaita kwa jina (Pemba) la huko kwao ili kutosahau walikotoka (Mwashota, 2019).

Aidha, wakati tunakusanya data wilaya ya Mtwara Vijijini tulikuta eneo linaloitwa Pemba. Eneo hilo lipo katika kata ya Naumbu. Baadhi ya watoataarifa walisema kuwa hapo kale eneo hilo liliitwa Pemba-Pwani kwa lengo la kulitofautisha na eneo jingine lililoitwa Pemba huko Mikindani. Pemba ya Mikindani palikuwa pakilimwa mkonge. Kwa upande wa Mtwara, eneo linaloitwa Pemba ni hilo tu lililopo kata ya Naumbu Mtwara Vijijini. Baadhi ya watoataarifa walisema kwamba jina Pemba limetokea Msumbiji ambako kuna mji unaoitwa Pemba. Waliendelea kusema kwamba hata jina la Pemba iliyopo Zanzibar lilitokea Msumbiji. Watu walitokea sehemu inayoitwa Pemba Msumbiji kila walipofika walipaita kwa jina la kwao.

Kwa upande mwingine Hans (2014: 91) ameelezea kuhusu kisasili kinachozungumzia asili ya jina la Pemba kama ifuatavyo:

Palikuwa na jahazi saba ziliuka, hatukujuwa zinatokea wapi lakini inasemekana ziliuka zinakwenda hija. Zilikwenda mpaka zikapotea njia, wakaanza kuulizana tunawa wapi? Nahoza wa jahazi ilokuwa usoni akamwambia Uledi, ebu kweyaa utizame tuwa wapi? Maana hatukujti tunapokwenda tunachaka kwenda Maka, pano tuwa wapi? Uledi akakweya mnogti akaita makurumani, akakweya akatizama Mashariki, akatizama Magharibi, akatizama Kusini akatizama na Kaskazi. Uledi akamwambia, hivi mpaka sasa sinakona kokoti sina ninachokiona isipokuwa upande wa Kaskazi nakona asari za mosi, kwa chini nakona asari za mosi basi nahoza we ebu! Pemba! Hebu pemba

⁴ Pemba Bay ni eneo lililoko nchini Msumbiji.

mosi ulee!... Nahoza pale ndo akapemba akenda zake, umbe kwa bahati ule mosi ulikuwa kishiwa. Unajuwa desturi ya vishiwa vyoti vinavya mvuke. Nahoza akatupa nanga akasema hivi! Mabaharia woti, pamoja na watu woti ichabidi sasa wakwejuu ufukuoni wakatafute kuni na maji lakini hapana ruksa kwenda peke yako mfatane wawiliwawili. Wakatoka wakaingia porini wakatafuta kuni wakatafuta maji wakaleta chomboni.... Hii ndiyo asili ya jina Pemba.

Katika kisasili hicho inaelekea asili ya jina la Pemba ni kutokana na watu waliokuwa wakisafiri kwa jahazi wakielekea Maka. Baada ya kupotea njia wakajikuta wanatia nanga katika kisiwa ambacho hivi sasa kinajulikana kwa jina la Pemba. Kwa mfano, kauli ya Uledi ya ‘pemba! Hebu pemba mosi ulee! Nahoza pale ndo akapemba akenda zake...’ katika maelezo ya Uledi maana ya jina pemba ni lenga. Tukiangalia katika *Kamusi ya Kipemba* iliyoandikwa na BAKIZA (2012: 107) maana ya ‘pemba’ ni kitendo cha kupata kitu kwa kutumia mbinu ya mzunguko au kupita njia ya mzunguko ili kufika pahali. Kwa ujumla, kisasili kilichotolewa hapo juu kama ilivyokuwa katika maelezo ya watoataarifa waliorejelewa hapo juu, tunapata picha kuhusu asili ya jina la Pemba. Hivyo, halitakuwa jambo la ajabu kuona wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba kuwa na ufanano kwa kiasi fulani na wazungumzaji wa Kimakonde.

4.2 Asili ya Jina la Makonde

Jina ‘Makonde’ linalotumika kurejelea jamii ya watu wanaozungumza Kimakonde, lilielezwa na watoataarifa mbalimbali ambao kimsingi ni wazungumzaji wa Kimakonde kutoka katika maeneo ya Msimbati, Msangamkuu, Mgao, Naumbu, Pemba-pwani, Mkungu, Mikindani, Magengeni, Kisungule na Mtanya ambako utafiti huu ulifanyika kuwa maana yake ni ‘pori’. Hii ilitokana na maeneo ya misitu waliyokuwa wanapitia wakati wa kuhama kwamba ilikuwa ni pori tupu. Hivyo, wakaitwa Wamakonde yaani watu wa porini. Hata hivyo, maana hiyo inatofautiana na ile inayotolewa na Rugemalira (2013) ambaye anasema kuwa “makonde” ni nomino yenyе maana ya jangwa/eneo kame au nchi kame. Wakati tunafanya utafiti maeneo ya Pemba, ilibainika kwamba katika Kipemba kuna neno ‘makonde’ lenye maana ya mashamba au ardhi na ‘konde⁵’ lina maana ya shamba. TUKI (2019) mbali na maana nyingine wanafasili neno *konde* kwa maana ya shamba lilitolimwa na kwamba kisawe cha konde ni shamba. Ukichunguza maelezo yaliyotolewa hapo juu utabaini kwamba kuna uhusiano wa maelezo yaliyotolewa Pemba na yale yaliyotolewa Mtwara kuhusiana na jina la Makonde na Konde. Ingawa kuna wanaotazama konde kwa maana ya pori na wengine kwa maana ya shamba, kimsingi maana hizi zinahusiana kwa kuzingatia dhana ya jumla ya kile kinachorejelewa.

⁵ Tazama pia, Shoup (2011: 179) anayeeleza visawe vingine vya jina “Makonde” kuwa ni Chimakonde, Konde, Maconde.

4.3 Chimbuko la Wapemba

Kwa kuzingatia utafiti uliofanyika kisiwani Pemba, kuna maelezo mbalimbali yaliyotolewa na watoataarifa kuhusu chimbuko la watu wa Pemba. Mathalani, tulipokuwa tunafanya utafiti maeneo ya Shamiani, mtoataarifa mmoja alieleza kuhusu chimbuko la watu wa Pemba kwa kueleza kwamba baba yake alitokea maeneo ya Mtende-Makunduchi wakati mama yake alitokea Unguja sehemu za Matembwe. Baba yake alitokea Makunduchi mpaka Unguja⁶ hatimaye bandari ya Kihimbili iliyopo Pemba. Katika matembezi yake ya Kengeja na maeneo mengine mtoa taarifa huyo akapendezwa na kisiwa cha Shamiani kilichopo ng'ambo ya Kengeja akawajulisha watu aliowakuta kwamba "Jamani mimi shamia huku (nahamia huku)". Kutokana na maneno 'shamia huku' ndipo likazuka jina la eneo la Shamiani. Mtoataarifa huyu alieleza zaidi kuwa baada ya watu hao kuzaliana, baadhi ya ndugu na jamaa walihamia Kengeja na wengine wakabaki Shamiani. Aliendelea kueleza kuwa mwanzoni, wake wa baba yake walikuwa wanaongea Kiunguja lakini baadaye wakaacha na kuanza kuongea Kipemba. Aidha, watoataarifa kutoka Shamiani walieleza kuwa watoto wao wanakijua Kipemba tu na sio Kimakunduchi wala Kiunguja, luga za mababu na mabibi zao hawazijui na hawawezi kuzizungumza.

Maelezo ya mtoataarifa huyu yanaonesha kuwa wakazi wa Pemba ni matokeo ya mchanganyiko wa watu amba ni wahamiaji kutoka katika maeneo tofautitofauti. Kwa mfano, tunaona kuwa kuna uwezekano kwamba wakazi wengi wa Pemba ni wahamiaji kutoka maeneo mbalimbali ya visiwa vy'a jirani. Visiwa hivyo ni pamoja na kisiwa cha Tumbatu⁷ na Unguja. Kwa mfano, baadhi ya watoataarifa wa Shamiani walisema kwamba wengi wao wameoa kisiwa cha Tumbatu.

Kwa upande wa Kojani baadhi ya watoataarifa walisema kuwa maana ya Kojani ni koo tofautitofauti kutoka katika sehemu mbalimbali. Watoataarifa hao walisema pia kuwa, waanzilishi wa Kojani walikuwa ni wazee wawili waliotokea maeneo ya Gombehume na Chamanangwe yaliyopo Wete baadaye wakaja watu kutoka maeneo mbalimbali kama vile Tanga, Komoro na Lamu. Pia, ilidaiwa na watoataarifa hao kuwa kuna sehemu katika visiwa vy'a Komoro inayoitwa Kojani. Sehemu hiyo ndiyo inayokaliwa na watu kutoka Kojani. Kuna watoataarifa wengine kutoka sehemu hii waliodai kuwa wao ni Wagunya kwa asili wanaotokea Mombasa, Kenya na mpaka hivi sasa bado wana udugu na watu wa Mombasa na Lamu na kwamba ikitokea misiba huwa wanakwenda mpaka Lamu kwenye shughuli za mazishi.

Mbali na udugu baina ya Wapemba na Wagunya kama unavyoelezwa na baadhi ya watoataarifa wa Kojani, katika maeneo mengine kama vile Kisiwa cha Panza walisema kwamba chimbuko la watu wa Pemba ni wavuvi kutoka maeneo

⁷ Hata hivyo, Tumbatu huchukuliwa kama kisiwa kidogo cha upande wa Unguja.

mbalimbali ya Tanzania Bara, Kenya na kwingineko. Wavuvi hao walifika kisiwani hapo kutokana na upepo wa bahari kuwapeleka kule ambako hawakupanga kwenda. Tulipouliza zaidi maana ya ‘Panza’ walisema kwamba neno hili lina maana ya *kwanza* kwa maana kwamba ni kisiwa cha *kwanza* kugundulika na kupendwa na wavuvi walioweka makazi yao mahali hapo.

Watoataarifa kutoka Kisiwa Panza walisema kuwa katika Kisiwa hicho, wavuvi hao walionekana kutokea katika maeneo mbalimbali ya pwani baada ya wao kuhamia mahala hapo na baadaye walizaliana. Baada ya kuzaliana walijikuta wakijigawa katika makundi matano tofauti. Makundi hayo ni matokeo ya ugomvi mionganoni mwao uliowasababisha kutengana. Kutokana na ugomvi huo kuendelea kwa muda mrefu, kuna mti ujulikanao kama ‘mpanda’ ambaao ulimea. Mti huo una matawi matano tangu ukiwa mdogo mpaka sasa. Kadiri siku zilivyozidi kusonga mbele, mgogoro uliokuwapo baina yao ulianza kupungua kwa sababu ya mti ulioota ukiwa na matawi matano ambaao uliwafanya waamini kuwa wao ni wamoja.

Mtoataarifa mwingine kutoka kisiwa Panza alisema kuwa baadaye wakazi wa Kisiwa Panza walianza kwenda kutambika katika mti huo yaani ‘Mpanda’ kutokana na mwonekano wake kuwa wa ajabu waliona kuwa chini ya mti huo kuna Mungu. Katika masimulizi yao, baadhi ya watoataarifa walidai kuwa katika miaka iliyopita ilikuwa haiwezekani kuupiga picha mti huo kwa sababu mahali hapo palichukuliwa kuwa mahali pa matambiko. Kila aliyepiga picha, mti huo haukutokea pichani. Kilitokea kivuli tu ambacho hakioneshi chochote. Kutokana na mwingiliano wa watu wa jamii mbalimbali, watu wa Kisiwa Panza wameacha kutambika katika mti huo na sasa picha zikipigwa zinatokea.

Aidha, kuna watoataarifa kutoka Shamiani waliodai kuwa wao wanatokea katika maeneo ya Makunduchi. Walidai kuwa mababu zao walifika mahali hapo kutokana na sababu mbalimbali kama vile njaa, migogoro ya kifamilia au baina ya jamii moja na nyingine, kodi ya kichwa na nyinginez. Kuna watoataarifa wengine katika kisiwa cha Shamiani waliodai kuwa chimbuko lao ni kutoka Uganda ingawa wamesahau kabisa lugha yao kutokana na muda mrefu kupita wa kutokwenda kwao. Walisema kuwa kwa sasa wao wanazungumza tu Kipemba.

Juma (2011) kwa upande wake anafafanua chimbuko la watu wanaoishi maeneo ya Wete kuwa ni mchanganyiko kutoka vijiji mbalimbali nya Pemba, watu wenye asili ya Asia na maeneo mengine nje ya Pemba. Hata hivyo, Juma (keshatajwa) hajaweka wazi makundi ya watu wanaotokea nje ya Pemba pengine ni kutokana na mawanda ya utafiti wake. Juma (2011) anaeleza zaidi kuwa watu wa Wete wana utamaduni mchanganyiko kwani upo utamaduni unaopatikana sehemu za bara, na pia kuna utamaduni wa kigeni, kama vile wa Kiarabu na Kiajemi. Maelezo ya Juma kuhusu mchanganyiko wa utamaduni wa watu wa Pemba yanashadidia suala la kuwapo kwa watu wa jamii mbalimbali maeneo ya Pemba ambaao ndio chanzo

cha upatikanaji wa tamaduni tofauti. Maelezo ya Juma (2011) yanadhihirisha pia kuwa kuna uwezekano mkubwa wa uhusiano wa kihistoria na namna nyingine wa watu wa Pemba na jamii nyingine za Bara.

Aidha, tukirejelea kisasili kilichotolewa na Hans (2014) kuhusu asili ya jina Pemba kuna madai kuwa eneo hilo huko nyuma lilikuwa ni pori tu halikuwa na watu. Kama hivyo ndivyo, kuna uwezekano mkubwa kwamba wakazi wengi wa mwanzo wa Pemba ni wageni kutoka maeneo mbalimbali waliojongea katika kisiwa cha Pemba kutokana na sababu mbalimbali. Hoja kwamba kisiwa cha Pemba kina mchanganyiko wa watu kutoka sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tanzania Bara na Kenya, imewahi kutolewa pia na Ghassany (2010: 112) anaposema:

Kihistoria sisi binadamu wananchi ni wamoja. Pemba kaskazini sana wametokea Tanga. Wadigo na sehemu za Lamu, huku Mombasa huku. Ukija kusini yake wengi wametokea Msumbiji. Ukenda kisiwa Panza pale ukiwakuta wazee wenye umri mkubwa ukimwuliza asili ya kabilia yake atakwambia Mmakonde, Mmakua, waliletwa na Mreno. Unguja hii Matemwe ni watu wenye asili ya Pemba Bay. Kuna kisiwa pale kinaitwa “Matemo” ndiko walikotokea. Ukifika Pemba Bay mjini pale ukiuliza “Matemo” utaambibiwa kisiwa kile pale wanatoka hapa ni Wamakua. Kivazi, tabia zao zote, vyakula wanavyotumia Matemwe ndivyo wanaotumia wale kule. Uwele, mtama, mhogo mkavu ule.

Chaaniasili yake ni Wamakonde wa Mtwara. “Chaani mwepo” Wawili wale walikuwa wanagombana. Sasa yule wa tatu akauliza “Chaani mwepo. Simgombana?” Nini nyinyi mnachogombana? Ndo neno “Chaani.” Chaani mwepo champatana” Akiwaliza hawa hawataki kujibizana wanagombana tu “e, nipamwanda.” Ndo ikawepo Donge Muwanda sijui na Chaani “Muwanda” maana yake “Mimi nenda zangu” hamnisikii, hamnijibu, mimi naondoka. Asili yao Wamakonde. Na ukienda pale Chaani masingini uliza maana ya “Chaani” kwa wazee watakwambia. Asili yao ni Wamakonde.

Kwa kuzingatia maelezo ya Ghassany ni dhahiri kwamba imebainika kwamba chimbuko la watu wa Pemba ni kutoka katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tanzania bara na Msumbiji. Imebainika pia kwamba, watu wa Msumbiji walio wengi walikwenda Pemba wakati wa utawala wa Mreno. Mbali na Wamakonde kuwapo Pemba, katika maelezo ya Ghassany (keshatajwa), inaonekana kuwa Wamakonde pia wapo Unguja katika maeneo ya Chaani. Nao walijongea katika maeneo ya Pemba na kwingineko kutokana na sababu mbalimbali za kihistoria, kiuchumi kama vile kutafuta riziki katika shughuli za kilimo.

4.4 Chimbuko la Wamakonde

Tulipokuwa tunafanya utafiti mkoani Mtwara katika wilaya ya Mtwara Vijijini na Manispaa ya Mtwara-Mikindani, watoataarifa walio wengi walisema kuwa asili

yao ni Msumbiji katika eneo moja linalojulikana kama Ndonde kupitia mto Ruvuma. Mathalani, mmoja wa watoataarifa katika kijiji cha Mkungu alisema kuwa:

“Hiki kijiji kimekuja na watu watatu; Amri bin Mwanya, Seleman bin Mwanya na binti Mwanya. Hawa wametoka Luli Msumbiji. Ikawa wamepita mwoote humo Msimbati wakakataliwa kwa sababu walikuwa na watumwa. Watumwa walikuwa kama mia tatu na kitu hivi. Wakafika Msimbati wakakataliwa wakasema hapa hakuna nafasi wakafika Mkubilu hakuna nafasi wakafika Msanga Mkuu hapo hakuna nafasi, wakavuka Mtwara hapa. Hapa wakakaa kidogo Mtwara wakaona eeh yale maji yapo karibu na maji mengi sasa wakaogopa watapoteza watoto. Ndio kuhama kuja Viseti hapana kitu, wakafikia hapo Pemba hapana chochote. Ndio moja kwa moja mpaka Naumbu. Walipofika Naumbu ndio wakaambiwa huku kuna sehemu moja Bandari yaani wanatoka watu bara wanakuja kuvua tu na kurudi. Unaona wale ndio kuja hapa tena wakafikia hapa wakaujenga mji kulee kukaitwa Makua. Ndio asili ya mji huu. Wamepakuta hapa hapakai mtu, hapana chochote kile wao ndio wakaanzisha kijiji. Jina Mkungu walipanga tu wenyewe. Asili ya mji huu Makua. Na kabilia lao Wamakua sio kabilia jingine. Waarabu hapa hawajaishi, wameishi Mikindani. Kwa kutembea walikuwa wanatembea kwa sababu wazee wa hapa ilikuwa na wao walianzisha hao walifanya biashara hiyo kwenda bara wakakusanya watu wawili watatu wakapeleka Mikindani kuja kuwauza”.

Katika maelezo hayo ya watoataarifa imebainika kuwa wakati watu wanatoka Msumbiji kwenda maeneo mbalimbali ya Mtwara, tayari kulikuwa na watu. Hata hivyo, hakuna ufanuzi wa kina uliotolewa na watoataarifa kuhusu kabilia walilolikuta katika maeneo hayo waliyokuwa wanapita. Pia, watoataarifa hawakutoa tarehe maalumu ambayo watu hao walihamia katika maeneo hayo.

Mbali na mambo mengine watoataarifa kutoka Msimbati wanaeleza kuwa wakazi wa Msimbati kiasili pia wanatokea Msumbiji. Hoja hii inaweza kutazamwa kupitia katika dondo lifuatato kutoka kwa mtoataarifa mmoja kutoka Msimbati kama ifuatavyo:

“Walioanzisha kijiji hiki sana sana ni watu wawili wametembea walikotembea huko baharini wakaona ule pale nlima lakini watu tafauti yao watu wawili hao utofauti kila mmoja amekuja kwa pake. Unafahamu walipokuja nlima wa kwanza yule akizungukazunguka akaona hapa mahala ni pazuli akanogewa. Akarudi akaenda akajipanga jina lake Ngosi na wa pili jina lake ni Sharif lakini hawa wametoka miji tafauti. Wa kwanza huyu katika kufika kwake amefikia kusini huku na huyu wa pili katika kuja kwake akafikia kaskazini. Hawajuani hao. Sasa kila mmoja ana hamu ya kuzunguka hapa mahala eeh wamezunguka wamezunguka haa! Wamekutana.

Habari! Njema! Salama salama! Wewe nani? Mimi Ngosi. Ahaa sawa umetokea wapi? Nimetokea Msumbiji. Wewe nani? Mimi Sharif. Umetokea wapi? Natokea sehemu hizi za Manga⁸ hizi. Sawa. Sasa wewe mwenzangu unasemaje? Mwenzangu, mimi mwenzio nimekuja nikazunguka kisiwa hiki nikannogewa nikarudi kujifunga ili nifanye makazi hapa. Basi ulivyofanya wewe nami nataka kufanya hivyo hivyo hivyo eeeh. Wewe fanya makazi sehemu yako iyo nami nafanya makazi sehemu yangu. Ikawa hivyo, Ngosi akawa na makazi yake na huyu... Lakini kwa jambo lolote lile litalokuwa limetutokea eee watu sisi inabidi tushirikiane likiwa la kheli likiwa mbaya eeeh hilo utakaloona jambo itabidi tuelezane. Wameishi ivyo eeeh huyu akiwa na jambo, akiona jambo anampelekea taarifa mwenzie na yule akiona jambo anampelekea. Hivyo mpaka ikafikia hatua ya kuzaana. Kwa kuzaana huyu aliyefika kwanza huyu huku alikuwa na familia nyingi akaanza majenzi, ujenzi kule na nji kubwa ikawa nayo huyu baada ya siku na huyu akafuatia. Kwa hiyo ilikuwa hivyo na waanzilishi ni hawa niliokueleza”.

Maelezo hayo ya watoataarifa kutoka Msimbati yanaonesha kwamba katika kipindi cha nyuma, eneo la Msimbati lilikuwa halikaliwi na watu kabla ya ujio wa wageni na ndio maana inasemekana kwamba, Ngosi na Sharif ndio waanzilishi walioanzisha makazi ya mwanzo katika eneo hili. Awali, Ngosi na Sharif walikwenda katika eneo hilo la Msimbati bila familia zao lakini baada ya kuandaa makazi walirudi Msumbiji kuoa na kuanzisha familia. Yamkini wageni watatu na kundi la watumwa⁹ walipopita maeneo ya Msimbati watu waliowaambia kuwa hapana nafasi mahali pale (Msimbati) ni jamii ya watu kutoka Msumbiji iliyotokana na uzao wa Ngosi na Sharif.

Aidha, maeneo mengi hapo kale kabla ya ongezeko kubwa la watu, yalikuwa yakizungukwa na misitu tu. Kwa mfano, mtoataarifa mmoja kutoka Naumbu anasema:

Kwa historia haya maeneo zamani yalikuwa ni eneo kama la kawaida tu, misitu. Lakini baada ya kumalizika karne zile ambazo utumwa, kuwaachia watu huru basi kuna baadhi ya watu walitokea sehemu za Bwahali, Chitengwa ambako walikofikia watumwa wakasema pale mbona pana nchanga. Yaani wakafuata huu mchanga. Basi huyu anatoka huku kuja hapa kuhamia kufyekafyeka kakaa, akaja, anarudi jamani! Kule kuna sehemu inafaa sana kuhamia na kuna maji. Hivyo ndivyo walivyoanza kuangalia mustakabali mzima wa ardhi hii ilivyokaa. Basi wanakuja watu mmoja hadi mwингine mmoja hadi mwингine wanaooana, wanazaana mmoja hadi mwингine hadi kufikia sisi kukuta mababu wa mababu. Wapo walitokea Msumbiji na wapo walitokea sehemu za Makua...

⁸ Manga ni jina la mji uliopo Msumbiji.

⁹ Tazama pia Ali (2016)

Maelezo katika dondo hilo yanaonesha kuwa Wamakonde ni jamii ya watu waliotoka katika maeneo mbalimbali ikiwemo Msumbiji ambao wamekuwa wakihamahama kwenda huko na kule kwa ajili ya kutafuta mahitaji yao. Pia, maelezo katika dondo hilo ynadhahirisha kuwa mtandao wa biashara ya watumwa ulichangia kwa kiasi kikubwa kuhamahama kwa Wamakonde ambao walijikuta wakisambaa katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Pemba. Msambao huo wa Wamakonde unachangia kwa kiasi kikubwa kuwa na uhusiano wa kimnasaba na jamii nyingine kama vile Wapemba na wengineo. Ndio maana Liebenow (1971) anaeleza pia kuwa ni vigumu sana kufahamu muda maalumu ambao Wamakonde walihamia Tanzania Bara. Hata hivyo, kwa mujibu wa watoataarifa ambao ni wazungumzaji wa Kimakonde wanaeleza kuwa walihamia maeneo ya Tanzania Bara kati ya karne ya 18 mpaka karne ya 19.

Pia, kumbukumbu za kihistoria zinaonesha kuwa Wamakonde ni watu ambao asili yao ni Msumbiji na kwamba wamekuwa wakihama kutoka eneo moja hadi jingine kutokana na sababu mbalimbali kwa mfano, Manus (2010) kwa upande wake anasema kuwa, Wamakonde wanaaminika kuwa asili yao ni sehemu iitwayo Ndonde iliyopo kaskazini mwa Msumbiji. Anaendelea kufafanua kuwa kundi kubwa la Wamakonde lilihamia kusini mwa Tanzania Bara miaka ya 1700 mpaka miaka ya 1800. Manus anaeleza sababu ya kuhama kwa Wamakonde hao kuwa ilikuwa ni kukimbia utumwa wa kabilia la Wangoni nchini Afrika Kusini. Mbali na mambo mengine, kumbukumbu hizi za kihistoria zinadhahirisha kuwa Wamakonde ni mionganini mwa jamii za watu waliohama kutoka eneo moja hadi eneo jingine. Suala hilo la kuhamahama kwa Wamakonde lilihababisha jamii hii kuweka makazi katika maeneo mbalimbali ambayo waliona wanaweza kupata riziki ikiwa ni pamoja na Pemba ambako kwa mujibu wa watoataarifa, wageni hao waliona wanafanya kazi kwa amani huku wakipata ujira wao. Hali hiyo ilikuwa ni tofauti na ilivyokuwa Msumbiji ambako walikuwa wakiteseka katika mashamba ya Wareno kwa kufanya kazi ngumu yenye ujira mdogo kama anavyooleza Manus (2010).

Naye Bonate (2007) anasema kuwa Kimakonde kimetokana na watu wa asili tofautitofauti mathalani wakimbizi kutoka kwenye utumwa. Watu hao waliungana na kuunda lugha moja inayojulikana kama Chimakonde huko uwanda wa juu wa Mueda¹⁰ katika karne ya 19. Hata hivyo uhalisia unaonesha kwamba Wamakonde walitumia lugha ya Kimakonde ambayo walikuwa wakiizungumza Msumbiji tofauti na madai ya Bonate (2007) Katika miaka ya 1950 idadi kubwa ya watu kutoka Kaskazini Msumbiji ilihamia Tanganyika, Zanzibar, Kenya na Malawi ‘Nyasa land’¹¹. Wengi wao walikwenda katika maeneo hayo kufanya kazi vijijini

¹⁰ Hili ni jina la wilaya mojawapo Msumbiji inayopatikana jimbo la Cabo Delgado.

¹¹ Kwa sasa nchi hii inaitwa Malawi, jina la Nyasa land lilitumika kipindi cha utawala wa Mwingereza.

kwenye mashamba ya mkonge. Baada ya mwaka 1954 jamii za Waingereza zilitoa sheria kuhusu vyama vya kijamii, wahamiaji hao wakaunda vyama/vilabu mbalimbali kama vile chama cha Wamakonde na chama cha Wamakua na Wamakonde katika miji ya Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar, Pemba, Morogoro na Mombasa. Chama cha Muungano wa Wamakonde wa Msumbiji Dar es Salaam ni chama kilichokuwa karibu sana na TANU. Waanzilishi wake walio wengi walikuwa na kadi za TANU walizozita “kadi¹² Chama Tanu” (Bonate, 2007).

Bonate anaeleza zaidi kuwa, mwaka 1961 chama cha TMMU kilibadilika na kuwa MANU (Mozambique African National Union) ili kuendana na chama cha TANU. Rais wa chama cha MANU aliyejulikana kwa jina la Matheus Mmole alitokea Tanganyika. Katika kipindi hicho vyama vingi, kikiwemo MANU, vilikuwa chini ya TANU. Pia, ushiriki wa uongozi wa Matheus Mmole katika chama cha MANU kutoka Tanganyika, inaonesha namna Watanganyika na watu wa Msumbiji walivyoshirikiana kudai uhuru wa Msumbiji. Siyo tu kwamba watu wa Tanganyika walioshirikiana na Wamakonde wa Msumbiji kudai uhuru bali hata watu wa Zanzibar. Kwa mfano, mwaka 1961 Umoja wa Wamakonde na Wamakua waliokuwa wakiishi Zanzibar walikirejelea chama cha MANU kama Z-MANU.

Maelezo yaliyotolewa na Bonate (2007) yanapata usuli kuhusu jamii ya Wamakonde walivohama kutoka katika eneo lao la asili na kwenda katika maeneo mbalimbali ya pwani ya Afrika Mashariki na kwingineko. Maelezo hayo pia yamesaidia kushadidia hoja ya kwamba kwa hakika mpaka sasa jamii nyingi za Pwani zina mchanganyiko wa watu kutoka katika maeneo tofautitofauti. Kwa mfano, Bonate (2007: 242) anasema:

Simango¹³ alifika Zanzibar na Pemba mwezi Aprili 1963 na kuzungumza kwanza na chama cha ASP (Afro Shiraz Party) chama kilichokuwa na Wamakua, Wayao na wahamiaji wengine kutoka Msumbiji (Tafsiri na mabano ni yetu).

Kwa kurejelea maelezo hayo ni dhahiri kwamba hata watu wa Unguja na Pemba wakiwamo waliokuwa wafiasi wa ASP walitokana na mchanganyiko wa jamii mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali ya Msumbiji na Tanzania Bara, isipokuwa baadhi yao wanajinasibisha na wageni mbalimbali kama Washirazi kutokana na ukweli kwamba kuna uwezekano wa wao kuwa vizalia vya Washirazi. Kwa hiyo, ikabidi wajivishe uenyeji kama ilivyo katika maeneo mengi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwachano na Makutano ya lugha za Kibantu tunaona kwamba kuna wakati Wamakonde, Wapemba na Wamakunduchi wamewahi kukutana kutokana na sababu mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

¹² Cadi, neno hili kwa Kiswahili sanifu ni ‘kadi’. Hivyo basi, maana nzuri ya ‘cadi Chama Tanu’ ni Kadi ya chama cha TANU.

¹³ Jina la kiongozi mmojawapo wa harakati za kupigania uhuru wa Msumbiji.

Kwa ujumla, Wamakonde wanaelekea kuwa hawakuhamia tu Tanzania Bara, bali walihamia katika maeneo mengine pia ya visiwani kama vile Unguja, Pemba na kwingineko. Hii inatokana na shughuli mbalimbali za uvuvi na mambo mengine ya kutafuta riziki.

Suala la kuhama kwa Wamakonde kutoka Msumbiji na kwenda katika maeneo mengine kama vile Tanganyika na visiwa nya Zanzibar limeelezwa pia na Wemb-Rashid (1992) kuwa lilitokana pia na kukimbia mateso ya kulazimishwa kazi na Wareno. Kwa mfano, anasema kuwa Wareno walipoingia Msumbiji kwa mara ya kwanza katika kipindi cha karne ya 16 walikumbana na upinzani mkubwa katika maeneo ya pwani na bara. Anaendelea kusema kuwa baada ya Vita nya Pili nya Dunia, Wareno walianzisha mashamba makubwa ya mkonge na pamba kwa kutegemea wafanyakazi wa kuwalazimishwa '*forced labour*'. Wakati huo huo utawala wa kikoloni wa Tanganyika ulianzisha mashamba ya mkonge. Pia, huko visiwani Zanzibar (Unguja na Pemba) uongozi huo ulifungua mashamba ya karafuu na minazi. Wamakonde wa Msumbiji waliona bora kwenda kufanya kazi Tanganyika na visiwani Zanzibar ambako walau walikuwa wanalipwa badala ya kufanya kazi bila kulipwa chochote nchini kwao. Hivyo, tunaweza kusema kuwa Wamakonde hao walikwenda katika maeneo hayo kama wakimbizi.

Aidha, kuna utafiti uliofanywa na Nahonyo na wenzake (2005) kuhusu uharibifu wa viumbe vilivyopo katika misitu ya Pemba. Utafiti huo ulionesha kuwa mbali na Wapemba, kuna wahamiaji wa kutoka kusini mwa Tanzania ambao ni Wamakonde, na kutoka Tabora ambao ni Wanyamwezi waliohamia maeneo ya Pemba hususan Ngezi katika karne ya 20. Watu hao walikata misitu na kuanzisha mashamba ya mazao ya chakula. Wanasisitiza zaidi kuwa, miaka ya 1970 kuliibuka janga la njaa lililosababisha watu wengine kutoka bara kuhamia maeneo ya Makangale, Pemba hasa maeneo ya Ngezi kwa ajili ya kilimo.

Mbali na kulima huko, wanaeleza kuwa Wamakonde waliripotiwa kuwinda wanyama mbalimbali. Shughuli ya uwindaji wa wanyama iliyofanywa na Wamakonde inadaiwa kuwa, ilisababisha kupotea kwa wanyama mbalimbali. Kimsingi maelezo ya Nahonyo na wenzake yanaonesha kuwa Wamakonde waliohamia Pemba walikuwa wakifanya shughuli za kiuchumi nazo ni kilimo na uwindaji. Pia, utafiti wao unaonesha kuwa suala la watu wa Bara kuhamia visiwani Zanzibar lilikuwa endelevu katika kipindi hicho.

4.5 Uhusiano wa Kihistoria baina ya Wapemba na Wamakonde

Sehemu hii inaelezea uhusiano wa chimbuko la Wapemba na Wamakonde. Data za utafiti wa makala haya zinaonesha kuwa asili ya Wapemba na Wamakonde ni maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara, Msumbiji na kwingineko. Hii inatokana na ukweli kwamba wakati wa utawala wa Waarabu kuna kundi kubwa la watu lililokuwa linachukuliwa kutoka katika maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki

ikiwa ni pamoja na Tanzania Bara na kupelekwa Zanzibar. Kwa mfano katika data ifuatayo kutoka kwa mtoataarifa mmoja kutoka Mikindani Mtwara anasema:

Waarabu walipokuja hapa kitu kikubwa walichofanya ni biashara ya kununua watumwa bara na kuwaleta hapa (Mikindani) na kuwapeleka Arabuni. Hii ilikuwa kama stendi. Sasa wale Waarabu walipokuja walipokuta wenyeji hapa, walikuwa wanawatumia wale kwa sababu Mikindani kulikuwa na Mwaarabu ambaye alitangulia naye alikuwa Liwali wa Mjerumani akiitwa Mohamed bin Salim Nmmeta. Mohamed bin Salim Nammeta alikuwa Mwarabu. Sasa wale Waarabu wakitoka Maskat wanakuja Zanzibar. Pale Zanzibar wakifika wanaletwa huku kwa yule mwenyeji wao anawapokea, akishawapokea wale Waarabu waliochukua bidhaa kutoka Arabuni kuzileta huku. Sasa hapa yule Liwali anawajua watu, kamwite fulani! Kamwite fulani! Kamwite fulani hapa nimepokea wageni lakini nia yao kubwa wanataka watu wa kwenda kufanya kazi kule Arabuni ya kulima mashamba. Vitu ambavyo tunatumia kununulia ni shanga, simbi n.k. Wale watu wanachukua kutoka huku, wanapeleka bara. Kule wanakokwenda hawasemi kwamba sisi tunawataka hawa ni watumwa haaha wanasema tunawachukua kuna nafasi za kazi za kazi kule pwani. Sasa wanapokuja huku wanafikia pale. Wale Waarabu wanawapokea hawa wachukuaji wanapata hisa maalumu ya kwenda zao Arabuni wamawachukua wale wanawapeleka Arabuni. Kwa hiyo ilikuwa wanapatikana kwa njia hiyo siyo kwamba wanakwenda kupatana na mtu kama unavyokwenda kununua mbuzi au kuku, wanawadanganya kidogo. Kwa hiyo wanawapeleka kule Arabuni kwenda kufanya kazi.

Maelezo katika data hiyo hapo juu yanadhihirisha kuwa watumwa walikuwa wanatoka sehemu mbalimbali za Bara na kupelekwa Mikindani. Pia, inaelekea katika kipindi hicho Mikindani ilikuwa ni sehemu ya kukusanya watumwa kama vilivyokuwa vituo vingine kama vile Bagamoyo na Mombasa. Baada ya kuwakusanya watumwa hao walipelekwa hadi Zanzibar ambako ndiko kulikuwa soko kuu la watumwa.

Uhusiano mwingine wa kihistoria baina ya Wapemba na Wamakonde tunauona katika maelezo ya Bonate (2007) ambaye anaeleza kuwa kuna kiongozi wa Wamakonde kutoka Msumbiji anayejulikana kwa jina la Simango aliyekwenda Pemba, na maeneo mengine ya Zanzibar mwezi Aprili 1963 kwa ajili ya kuhamasisha suala la kupigania uhuru wa nchi yao ya Msumbiji. Katika maelezo yake inaonesha kuwa Wamakonde wameanza muda mrefu kuchangamana na watu wa Zanzibar tangu kipindi cha ukoloni hadi hivi sasa.

Katika maelezo ya Bonate (2007) anaeleza kuwa katika vyama vyaa kupigania uhuru vilivyokuwapo Zanzibar vilikuwa na wanachama ambaa ni Wamakonde, Washirazi na Wamakua. Maelezo hayo yanaonesha uhusiano wa kihistoria baina ya Wamakonde na jamii ya watu wa Zanzibar kuwa wameanza kushirikiana kwa

kipindi kirefu. Pia, mwingiliano baina ya Wamakonde na watu wa Zanzibar kama vile Wapemba ulielezwa na watoataarifa kuwa mpaka sasa bado wanaendelea kuingiliana hasa katika suala zima la ndoa. Kwa ufanuzi zaidi tunaona hata katika maelezo ya Heschel (2009) ambaye anaeleza kuwa:

Utamaduni wa Waswahili, wakazi wa pwani ya Afrika Mashariki si utamaduni wa namna moja au wa kabile moja. Ni matokeo ya utamaduni mchanganyiko wa mataifa na asili tofauti. Makabila ya Afrika yaliingiliana na wafanyabiashara wa Kiarabu waliofanya makazi yao Pwani ya Afrika Mashariki. Hivyo basi, biashara na kuoana ilisababisha kuibuka kwa lugha ya namna yake yaani Kiswahili hususah utamaduni wa Kiswahili. Pamoja na mchanganyiko wa kiutamaduni kila kabile linajibainisha kwa namna yake huku likiendelea kubadili mambo ya utamaduni wa wengine. Suala hili limekuwa endelevu (Tafsiri ni yetu).

Maelezo yaliyotolewa na Heschel (2009) yanaonesha kwamba watu wa pwani ya Afrika Mashariki wana tamaduni zao zilizotokana na matokeo ya mwingiliano baina yao na watu wa mataifa mbalimbali waliokuwa na makutano nao katika kipindi cha nyuma. Pia anaeleza kuwa suala la mwingiliano na kubadilika kwa utamaduni wa jamii fulani ni endelevu. Pengine ni kutokana na jamii za watu kuingiliana kila leo. Heschel (2009) anasisitiza pia kuwa biashara na ndoa ni mionganoni mwa mambo yaliyosababisha mabadiliko ya utamaduni wa jamii moja na nyingine.

Pia, biashara na ndoa ni masuala yaliyosababisha jamii moja na nyingine kuhusiana. Kwa mfano, Wamakonde waliohamia Zanzibar, mathalani, Pemba walipenda kuendeleza utamaduni wao wa kuwafunza wasichana na wavulana jando na unyago kama ilivyokuwa kawaida katika sehemu zao za Msumbiji walizotokea. Kutokana na watu waliowazunguka kutofanya jando na unyago walijikuta wakibadilika na kuwa na utamaduni mwingine wa kutowafanya jando na unyago vijana wao tofauti na jadi yao.

Ali (2016) anaeleza njia mbalimbali walizopita Wamakonde kwenda Zanzibar, mathalani katika kisiwa cha Pemba na kwingineko kwa kusema kuwa:

Wamakonde wengi waliohamia Pemba walihamia baada ya kufanya makazi baadhi ya sehemu wakati wakifanya kazi katika mashamba ya mkonge. Safari yao haikuwa ya moja kwa moja. Baadhi walikwenda kirasi kwa kupitia katika bandari ya Malindi (kwa waliokeea Mtware na Dar es Salaam) na Wete (kwa waliokeea Tanga). Wamakonde wengine waliokwenda Pemba kwa njia zisizo rasmi, wengi wao walitumia usafiri wa ngalawa na kupitia katika maeneo mbalimbali kama vile; Mtambwe, Wete na Mkoani. Kwa upande wa wale waliokeea Tanganyika walitaja maeneo mbalimbali walioyapitia ambayo ni pamoja na Tanga (Sakura), Kunduchi na Dar es Salaam.

Aidha, hakuna rekodi inayoonesha kuwa Wamakonde walitoka Msumbiji moja kwa moja na kwenda Pemba bila kupitia Tanganyika ili kupata “cheti cha njia”. Wamakonde wengi waliohamia Pemba walipoulizwa tarehe ya wao kufika Pemba, wengi walisema kuwa walifika Pemba kabla ya mika ya 1940 na 1960.

Maelezo hayo yaliyotolewa na Ali (2016) yanaonesha kuwa kuna Wamakonde waliohamia kutoka Msumbiji na kwenda Pemba na maeneo mengine ya Unguja kwa kupitia katika maeneo mbalimbali ya Tanganyika katika miaka ya 1940 na 1960 kabla ya uhuru. Pia, inaelekeea kuwa Wamakonde hao walipitia katika maeneo mbalimbali baada ya kutoka Msumbiji. Baadhi walipitia Tanga na wengine walipitia Kunduchi na Dar es Salaam. Vilevile, uhusiano mwengine wa kihistoria baina ya Wapemba na Wamakonde tunauona küpitia mtoataarifa wa Ali (2016:85) ambaye anaeleza kuwa:

Ninathubutu kusema kwamba, mimi ni kizazi cha mwisho cha Wamakonde waliopo Pemba, mwanangu wa kiume amesahau kabisa Kimakonde. Nikiwa ninazungumza Kimakonde ananielewa, lakini anashindwa kunijibu kwa Kimakonde matokeo yake anatumia Kiswahili.

Maelezo ya mtoataarifa huyo ynaonesha suala la mwachano linapoanza kutokea hususani mtu anapokosa watu wa kuzungumza nao inakuwa ni vigumu kuhamisha lugha aliyonayo suala lililokifanya kizazi chake kutumia zaidi lugha ya jamii ambamo wanaishi. Kwa upande mwengine, maelezo ya mtoataarifa huyo yanatoa uwezekano wa wazungumzaji wengi waliopo Pemba kuzungumza lahaja/lugha tofauti na za chimbuko lao walilotokea. Hoja hii inathibitika küpitia maelezo ya Ali (2016) anaposeema:

- Makundi matatu ya Wamakonde waliopo Pemba ni:
- (a) Wahamiaji wa Kimakonde ambao bado wana uhusiano na ndugu zao waliopo Msumbiji na bado wana mawasiliano ya karibu ingawa wengi wao hawajawahi kutembelea Msumbiji kwa kipindi cha miaka mingi.
 - (b) Wahamiaji wa Kimakonde ambao hawana uhusiano na ndugu zao waliopo Msumbiji. Kundi hili la Wamakonde huona Pemba nyumbani kwao.
 - (c) Vizalia wa Kimakonde ambao hawajui lolote kuhusu Msumbiji na hujinasibisha na Pemba kuliko Msumbiji. Wamakonde hao hujisikia vizuri kuitwa Wapemba kuliko kuitwa Wamakonde. Kundi hili halina alama yoyote inayowatofautisha na wenyeji.

Kwa ujumla makundi hayo matatu yaliyobainishwa na Ali yanadhihirisha uhusiano wa kihistoria baina ya Wapemba na Wamakonde ikiwa ni pamoja na mwingiliano walio nao uliosababishwa na makutano yao. Hata hivyo, makundi ya Wamakonde wa Pemba wasiohusiana na Wamakonde wa Msumbiji wanaonekana kuwa wengi kuliko wale walio na mawasiliano na ndugu zao ingawa hawajawahi kutembeleana. Waswahili husema fimbo ya mbali haiui nyoka. Hii inadhihirisha

ya kwamba Wamakonde hao wanahusiana kwa ukaribu na Watu walio Pemba kuliko wenzao walio Msumbiji.

5.0 Hitimisho

Makala haya yamejadili uhusiano wa Wapemba na Wamakonde kwa hoja za kihistoria ambapo imebainika kuwa kuna uhusiano wa karibu baina ya wazungumzaji wa jamii hizi kutokana na ushahidi wa mitandao ya kibiashara, kumbukumbu za kihistoria, maeleo ya wazungumzaji wa Kipemba na Kimakonde na uhusiano wa kimnasaba. Aidha, imebainika kwamba Wapemba na Wamakonde waliwahi kukutana kwa sababu katika kipindi cha wakoloni mathalani Wareno kuna kundi kubwa la Wamakonde waliohamma kutoka Msumbiji kuelekea katika maeneo ya mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Pemba na kwingineko kwa sababu ya ukatili wa Wareno na utoaji wa ujira mdogo kwa wafanyakazi katika mashamba ya mkonge. Pia, imebainika kuwa Wamakonde kwa asilimia kubwa ni watu waliokimbia vita na kuelekea sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Pemba ambako baada ya uhuru wa nchi ya Msumbiji baadhi yao walikuwa na tabia ya kurudi Msumbiji kwa ajili ya kusalimia jamaa zao¹⁴. Hivi sasa vizazi vilivyopo kwa kiwango kikubwa vinajinasibisha na jamii iliyopo kwa kuogopa kutengwa. Vilevile, Wamakonde waliotoka Msumbiji waliacha jina la eneo huko Msumbiji linaloitwa Pemba. Hivyo basi kwa kuwa walikuwa wana tabia ya kuita jina la kwao eneo walilohamia kuna uwezekano mkubwa wa kwamba jina Pemba kutokana na Wamakonde waliotoka Msumbiji kwa sababu mpaka sasa hakuna ushahidi wa wazi unaowaeleza Wamakonde wa kwanza kufika Pemba.

Kwa kuzingatia uhusiano uliobainishwa baina ya wazungumzaji wa Kipemba na Kimakonde utafiti mwingine unaweza kufanyika ukihuisha jamii hizi na jamii nyingine za wazunguzaji wa lugha nyingine tofauti na Kimakonde. Hii inatokana na sababu za kwamba wanazuoni alio wengi wameeleza kuwa Pemba kuna mchanganyiko wa jamii mbalimbali za watu waliotoka maeneo ya nje na Pemba. Pia, tunaweza kutazama uhusiano baina ya lahaja nyingine kama Kimakunduchi na lugha nyingine za kijamii au kuhusisha lugha nyingine za kijamii na lahaja nyingine za Kiswahili ili kuona uhusiano wake wa kihistoria na pengine kiisimu.

Marejeleo

- Ali, A. (2016) *A History of Makonde Migration to Pemba 1890- 1963*. Tasnifu ya Umahiri. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- BAKIZA (2012) *Kamusi la Lahaja ya Kipemba*. Nairobi: Oxford University Press.
- Beeks, R. S. P. (2011). *Comparative Indo-European Linguistics*. Philadelphia: John Benjamin Publishing Company.

¹⁴ Tazama Bonate (2007) na Ali (2016)

- Bonate, L. J. K. (2007) *Traditions and Transitions: Islam and Chiefship in Northern Mozambique 1850-1974*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Cape Town, Cape Town.
- Bowern, C. na Evans, B. (Wah.) (2015) *The Routledge Handbook of Historical Linguistics*. New York: Routledge.
- Chami, F. A. (Mh.) (2009) *Zanzibar and The Swahili Coast From c30, 000 Years Ago*. Dar es Salaam: E&D Vision Publishing
- Chum, H. (1994) *Msamiati wa Pekee wa Kikae*. Uppsala: Nordic Association of African Studies.
- Creswell, J. W. (2014) *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches*. New Delhi: SAGE Publications India Pvt. Limited.
- Enon, J. C. (1998) *Educational Research Statistics and Measurement*. Kampala: Department of Distance Education: Makerere University.
- Fox, A. (1995) *Linguistic Reconstruction: An Introduction to Theory and Method*. New York: Oxford University Press.
- Ghassany, H. (2010) *Kwaheri Ukoloni, kwaheri Uhuru! Zanzibar na Mapinduzi ya Afrabia*. United States of America: Washington DC.
- Greenberg, J. (1995) *Studies in African Linguistics Classification*. Connecticut: New Haven.
- Guthrie, M. (1948) *The Classification of Bantu Languages*. London: OUP.
- Guthrie, M. (1967) *Comparative Bantu*. Juz. 1 Farnborough: Gregg International Publishers.
- Guthrie, M. (1970a) *Comparative Bantu*. Juz. 2 Farnborough: Gregg International Publishers.
- Guthrie, M. (1970b) *Comparative Bantu*. Juz. 3 Farnborough: Gregg International Publishers.
- Guthrie, M. (1971) *Comparative Bantu*. Juz. 4 Farnborough: Gregg International Publishers.
- Hans, M. M. (2014) *Mchango wa Lahaja katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Sanifu: Hazina Fiche iliyomo katika Lahaja za Kiswahili za Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Heine, B. na Nurse, D. (wah.) (2008). *A Linguistic Geography of Africa: Cambridge Approaches to Language Contact*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Henschel, J. (2009). *Bagamoyo Where Cultures Met: History of the Town: A Guide to the Catholic Museum*. Bagamoyo: Desk Top Production Limited.
- Hock, H. H. na Joseph, B. D. (1996) *Language History, Language Change and Language Relationship: An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*, New York: Mouton de Gruyter.
- Juma, H. K. (2011) *Tofauti za Kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili cha Wete katika Kisiwa cha Pemba*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

- Liebenow, J.G. (1971) *Colonial Rule and Political Development in Tanzania: The Case of the Makonde*. Evanston: Northern University Press.
- Luraghi, S na Bubenik, V. (2010) *Continuum Companion to Historical Linguistics*. New York: Continuum International Publishing Group.
- Manus, S. (2010) "The Prosody of simákonde Relative Clauses." *ZAS Papers. Katika Linguistics*. Juz. 53: 159-185.
- Massamba, D. P. B. (2002) *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Massamba, D. P. B. (2007) *Kiswahili Origins and the Bantu Divergence-Convergence Theory*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mwashota, P. (2019) *Uhusiano wa Kimsamiati na Kihistoria baina ya Kipemba, Kimakunduchi na Kimakonde na Mchango wake katika Maendeleo ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamivu. (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Nahonyo, C. L, Mwasumbi, L. B, Msuya, C. A, Masao, C.A, Suya, T. B, Shing'wenda, C. (2005) *Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Care Tanzania and Department of Commercial Crops, Fruits and Forestry: Ngezi-Vumawimbi Forest Reserves Biodiversity Inventory Report*. Department of Zoology and Marine Biology: University of Dar es Salaam.
- Nurse, D. na Spear, T. (1985) *The Swahili: Reconstructing the History and Language of An African Society*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Nurse, D. na Hinnebusch, T. J. (1991) *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. Los Angeles: University of California.
- Nurse, D. (1997). "The Contributions of Linguistics to the Study of History in Africa." Katika *The Journal of African History*. Juz. 38: 359-391. Cambridge Univeristy Press.
- Rugemalira, J. M. (2013) *Kamusi ya Kimakonde-Kiingereza-Kiswahili*. Dar es Salaam: Mradi wa Lugha za Tanzania.
- Shoup, J. A. (2011) *Ethnic Groups of Africa and the Middle East: An Encyclopedia*. England: Oxford.
- TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (toleo la 4). Nairobi: Oxford University Press.
- Wemba-Rashid, J. A. R. (1992) *Vulnerable Groups Among Refugee Communities Experiences from Mozambican Makonde Children in Tanzania*. Nairobi: Institute of African Studies, University of Nairobi.